SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI KWA WAATHIRIKA
**WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU** 2023

TUME YA KIMATAIFA YA
**HAKI ZA BINADAMU**

JESHI LA WOKOVU

# NIMESIKIA VILIO VYAO



## MISAADA KWA WATOTO

Imeandikwa na **Meja Sandra Pawar**
*Teritori ya Marekani kusini*

### UTANGULIZI

ZULIA LA NDOTO:
Hadithi ya Ravi

Hii ni hadithi ya kweli. Jina langu ni Ravi*. Nafikiri niko kati ya miaka 12 na 13. Nilipokuwa mdogo, mtu alikuja kijijini, kwetu. Alikuwa anamtafuta mtoto wa kumfanyia kazi – kutengeneza mazulia kwa mkono. Aliwazungumzia wazazi wangu kwamba nitalipwa mshahara mzuri. Sikutaka kutoka nyumbani kwetu na mwanzoni, wazazi wangu hawakukubaliana naye. Lakini mtu huyu hakuwa tayari kupewa jibu la hapana. Mwishowe wazazi wangu walisalimu amri kwa matakwa ya huyu mtu. Yule mtu akawapa dola 10 anichukue. Lakini alikuwa amesema uongo. Sikulipwa kitu. Bado nakumbuka safari ya treni kwenda nyumbani kwa huyu mtu. Safari nzima alikataa kunilisha. Ilikuwa ni wakati tulipofika tulikokuwa tunakwenda ndipo aliponipa chakula kidogo nile. Siku iliyofuatia niliamka na tena, sikupewa chakula. Kisha yule bwana akanipeleka mahali palipokuwa na mashine za kufumia.

Hiyo ndiyo ilikuwa mara ya kwanza kuona mashine ya kufumia. Kutoka siku yangu ya kwanza, nililazimishwa kufanya kazi. Nililazimika kukaa kwenye mashine ya kufumia na kama nilishindwa kumaliza mchana, nilitakiwa kufanya usiku kwa mwanga wa mshumaa. Nililazimishwa kufanya kazi kwa masaa mengi, kwa hiyo sikuweza kupata usingizi wa kutosha, na kwa sababu nilikuwa siku zote nimechoka, nilifanya makosa. Sikupata fedha yoyote lakini nilipata kitanda. Sisi sote tulilala na kufanya kazi katika chumba kimoja na tulilazimishwa kufanya kazi hapo kwa masaa 12 kwa siku. Mara moja kwa siku tuliruhusiwa kutumia bafu lakini hata muda wa kwenda bafuni ulisimamiwa.

Tulipewa chakula kidogo sana – mara nyingi wali kidogo. Hatimaye, mimi niliponywa katika uvamizi uliofanywa na polisi. Niliogopa sana. Nilifikiria ninakwenda kupigwa tena na watanitupa mbali. Kwa bahati, nilipelekwa mahali ambapo watoto wanatunzwa. Napapenda hapa. Nina marafiki, ninafurahi na kwenda shule. Wanasaidia kufanya kieleweke kile kilichotokea kwangu – kwamba

*Jina limebadilishwa ili kumlinda.*

nilikuwa mtumwa. Sasa ninajaribu kujifunza niwe fundi umeme. Napenda wazo la umeme. Ndoto yangu ni kuwafundisha kaka zangu, dada zangu na kila mmoja kijijini kwangu.



## WAZO KUU

***Ni nini maana ya kuwa mtumwa au kuwa utumwani?***

Utumwa sio wazo jipya. Ni jambo ambalo limekuwepo kwa miaka maelfu mengi na hata tunasoma habari zake katika Biblia tunapojifunza historia ya Wayunani, Warumi na Wamisri na jinsi ambavyo wote walikaa na watumwa. Leo bado kuna watu wengi ambao wamo utumwani. Kwa kweli, wanafikiria panaweza pakawa na zaidi ya watumwa milioni 49.6 duniani hivi sasa. Hao ni wengi au siyo?

### MASWALI YA KUJADILIANA

- **Unafikiri mtu anajisikiaje akiwa mtumwa?**
- **Unafikiri Ravi (katika hadithi hapo mwanzo) alijisikiaje kuwa mtumwa na kutengwa na familia yake na kijiji chake?**
- **Unafikiri Mungu anawajali watumwa na wale walio utumwani? Kwanini au kwanini hapana?**
- **Unafikiri ni vema tuwajali watumwa na wale walio utumwani? Kwanini au kwanini hapana?**
- **Watumwa mara nyingi huwekwa katika hali inayowa**fanya wajisikie wana woga na hawako salama na mara nyingi wanafanywa wajisikie kuwa hawana faida nao sio watu muhimu. Wanalazimishwa kufanya mambo ambayo sio haki na magumu na yanayowaumiza. Wanaweza wakajisikia vile vile kwamba hakuna anayesikia vilio vyao au anayeelewa wanapitia yapi. Wanaweza kujisikia wako peke yao na wenye huzuni.

Kwa shukurani twatambua kwamba Mungu anawajali nao ni muhimu kwake. Anawapenda kwa kina na anasikia vilio vyao vya huzuni. Tunaweza kusoma kitabu cha Kutoka katika Biblia kwamba Mungu anajali naye anasikia. Katika Kutoka 2:23-25 inasema: 'Hata baada ya siku zile nyingi mfalme wa Misri akafa, wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa, wakalia, kilio chao kikafika juu kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa. Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake alilolifanya na Ibrahimu na Isaka na Yakobo. Mungu akawaona wana wa Israeli, na Mungu akawaangalia.'

### MASWALI YA KUJADILIANA

**Vifungu hivi vinasema nini kumhusu Mungu? Vinasema anafanya nini?**

Miaka yote hiyo maelfu iliyopita Waisraeli walipokuwa wanatendewa vibaya kama watumwa, Mungu alijali sana kuhusu hali yao. Katika dunia yetu leo anajali vile vile kuhusu mamilioni ya

**Upande wa kushoto:**
watu walio utumwani, wakubwa kwa watoto kama

Ravi ambao wanatendewa visivyo na ambao wanajiuliza kama kuna yeyote anayewajali. Vifungu hivi tunavyovisoma katika kitabu cha Kutoka vinatuambia kwamba hawako peke yao, na kwamba Mungu anasikia, Mungu anaona naye anaelewa.

**Upande wa kulia:**

Vile vile Mungu anatutaka sisi tuwajali wale ambao ni watumwa na wamenaswa utumwani. Anatutaka tufahamu kwamba zipo njia tunaweza kuzitumia kuwasaidia watu wanaotendewa vibaya.

---

## MASWALI YA KUJADILIANA

Una mawazo gani kuhusu kile tunachoweza kufanya? Baadhi ya mambo ambayo unaweza kufanya ni:

1. Fahamu ishara – jifunze ufahamu ni viashiria gani vinavyoweza kukuonyesha mtu fulani ananyanyaswa. Kuna mambo mengi ya kuangalia, ikiwa ni pamoja na hali za maisha ya watu, hali za kufanya kazi na kugundua jinsi watu wazima wanaowazunguka wanavyowatendea.

2. Jifunze namna ya kuwa salama mitandaoni – wewe na marafiki zako mnaweza kutunzana namna gani ili muwe salama?

3. Washirikishe wana familia na marafiki uliyojifunza leo na viashiria vya utumwa.

4. Jifunze zaidi kuhusu utumwa, usafirishaji haramu wa binadamu na unyonyaji. Shirikisha familia yako, marafiki zako na familia yako ya kanisani. Fanya uwasilishaji shuleni kwako au katika shule ya Jumapili.

5. Omba! Waombee watu wanaopitia utumwa, Mungu awalinde na asikie maombi yao. Waombee viongozi wetu na mashirika yanayowasaidia waathirika.

6. Watendee watu kwa wema, heshima na upendo.

7. Wahimize marafiki zako na wana familia wawatendee watu kwa heshima, wema na kwa upendo.

8. Waulize viongozi shuleni kwako na kanisani na hata katika serikali wawalinde na kuwasaidia vizuri zaidi watu ambao hawako salama.

---

# **Fahamu ishara** – jifunze ni viashiria gani vinavyoweza kukuonyesha mtu fulani ananyanyaswa

Hebu tuwaombee wale wote walio utumwani duniani na wanaotumikishwa kama watumwa.

*Mpendwa Yesu:*

*Tafadhali, wasaidie watumwa wote na wale walio utumwani duniani. Linda mioyo yao na akili zao. Wawezeshe wapate uhuru na wasaidie wapate usalama. Linda familia zao na saidia familia ambazo zimetengwa ziweze kurudiana tena. Wasaidie wafahamu unawapenda na unawajali na kwamba upo pamoja nao hata kama maisha ni magumu na yana huzuni. Wawezeshe wafahamu wao ni wa muhimu na wanapendwa.*

*Amina.*

Maombi kutoka kwa Alina, mwenye umri wa miaka 9 – yaliyotolewa kwa kibali ndani ya mfumo wa maadili ya utoaji hadithi.

## SHUGHULI

KIBANDIKO KILICHOGANDA

Katika eneo ambalo watoto wanaweza kuzurura/kukimbia huku na kule, mchague mmoja awe 'ndiye'. Wape watoto wengine sekunde 20 watoroke. Baada ya sekunde 20, mtoto ambaye 'ndiye' anaweza kukimbia akawawekee watoto wengine vibandiko. Watoto hawa hawataki kuwekewa kibandiko. Wakiwekewa kibandiko, wanatakiwa 'kuganda' (kusimama) mahali walipo na wainue mikono yao. Wawaite watoto wengine ambao hawajawekewa kibandiko wakimbilie chini ya mikono yao wawaondoe katika kuganda kwao wawaweke huru. Tunaweza kushirikishana haya katika maisha, tunataka kusikia vilio vya wale walio utumwani na tufanye pamoja nao na watu wengine wazima ili tuone wamewekwa huru kama tunavyofanya katika mchezo wa kibandiko cha kuganda. Kwa kutumia vikaratasi vya rangi

## KIBANDIKO KILICHOGANDA

KAZI YA MIKONO

mbalimbali, mtake kila mtoto achukue moja na aandike juu yake 'KOMESHA'. Kwa kutumia gundi, karatasi ya gundi au staple, unganisha vikaratasi vyote kutengeneza mnyororo wa karatasi ikiwa ni ishara ya kujitoa kwao na kanisa kusimama pamoja ili kukomesha utumwa. Hata unaweza ukafanya mashindano kuona ni nani anayeweza kutengeneza mnyororo mrefu zaidi. Ning'iniza mahali pako ili kumkumbusha kila mmoja katika majuma yajayo kwamba sisi tumejitoa kukomesha utumwa duniani.

